Ombi la Iowa Individual Disaster Assistance Grant Program (IIAGP)

MAAGIZO YA UKAMILISHAJI WA OMBI LA IIAGP

IIAGP inatoa ruzuku kwa familia ambazo mapato yake ya mwaka ya familia ni 200% au chini ya kiwango cha umaskini cha serikali kuu. Kila familia inayostahiki ***inaweza*** kupokea hadi $5,000.00.

Lazima familia zinazostahiki zitimize mambo yafuatayo:

- Mapato ya familia ya kila mwaka ni au chini ya 200% ya Kiwango cha Umaskini cha Serikali Kuu

KUMBUKA: Lazima mapato ya kila mwaka ya familia yawe 200% au chini ya kiwango cha umaskini cha serikali kuu kwa familia ya ukubwa huo.

Miongozo ya Umaskini wa Taifa 2023

Ukubwa wa Familia	1	2	3	4	5	6	7	8
200% ya Kiwango cha Umaskini cha Serikali Kuu (mapato ya kila mwaka)	$29,160	$39,440	$49,720	$60,000	$70,280	$80,560	$90,840	$101,120

- Wanafamilia ni raia au wanakaa nchini Marekani kihalali
- Makazi ya familia ya msingi yako katika kaunti iliyobainishwa katika udhibiti wa mkasa
- Familia ina mahitaji yanayohusiana na mkasa ambayo hayafidiwi kikamilifu na bima na hayakidhiwi na mpango mwingine wa msaada

Baada ya kuwasilisha ombi hili, tafadhali jitayarishe kutoa nyaraka zinazofuata unapoombwa:

- Utambulisho wa Picha
- Ithibati ya makazi halali nchini Marekani (Leseni, cheti cha kuzaliwa, pasipoti, Green Card, kadi ya ruzuku ya serikali, nk.)
- Ithibati ya mapato (hati za malipo, W-2, kodi ya mapato, barua ya ruzuku ya serikali, nk.)

- Nyaraka za bima (ikiwa zinahusika)
- Nakala ya mkataba wa kupangisha nyumba (ikiwa unapangisha)
- Picha za uharibifu (ikiwa zinahusika)
- Stakabadhi (ikiwa unaomba fidia kwa gharama inayohusiana na mkasa)
    - Ikiwa unaomba msaada wa ukarabati wa gari, ithibati ya usajili na bima ya dhima
- Uthibitishaji wa uharibifu wa mhusika mwingine unaweza kuombwa

Taarifa za Upotezaji Makao:

Kila familia inayostahiki ***inaweza*** kupokea hadi $5,000 kwa kila kipengee kinachostahiki chini ya moja ya kategoria nne zilizoorodheshwa hapa chini. Ikiwa unaomba fidia, lazima stakabadhi ziwe kwa jina la mwombaji.

1) Nyumba ya Muda Mfupi – Familia ***inaweza*** kupokea hadi $5,000 kwa kupangisha nyumba kwenye makao yenye leseni kama vile hoteli au moteli, ikiwa nyumba ya familia imeharibiwa, haiwezi kukalika, haiwezi kufikika, au haipatikani kwa familia. LAZIMA stakabadhi ziwe kwa jina la meombaji.
2) Msaada wa Chakula – Ubadilishaji wa chakula kilichooza au kilichoharibika.
3) Mali Binafsi – Baadhi ya mifano ni: vyombo vya jikoni, usafi binafsi, mavazi, samani na vyombo vya chumba cha kulala, nk.
4) Matengenezo ya Nyumbani – Baadhi ya mifano ni: utengenezaji wa sehemu za jengo, utengenezaji wa sakafu, kuta, madari, milango, madirisha na mazulia. Msaada utakataliwa kutokana na mambo yafuatayo: hali zilizopo ndizo chanzo cha uharibifu; jengo linalomilikiwa na mwenye nyumba; na ikiwa hatimiliki ya jengo haiko kwa jina la mwombaji.

Kuwasilisha Ombi:

Maombi yanapaswa kuwasilishwa kwa Community Action Agency yako ya karibu kwa barua au ana kwa ana, au yanaweza kuwasilishwa kielektroniki kupitia tovuti ya Department of Homeland Security and Emergency Management kwenye homelandsecurity.iowa.gov/assistance. Wasiliana na Community Action Agency yako ya karibu kwa mbinu nyingine za kutuma ombi ikiwa zinahitajika. Pata shirika lako kwenye www.iowacommunityaction.org/find-an-agency. Mtu mwingine kutoka Community Action Agency yako ya karibu atawasiliana nawe ili kukagua ombi lako. Jitayarishe kutoa nyaraka zitakazoombwa.

Kwa maswali, tuma barua pepe kwa IndividualDisasterAssistance@iowa.gov.

OMBI LA IOWA INDIVIDUAL DISASTER ASSISTANCE GRANT PROGRAM (IIAGP)

1. Taarifa za Mwombaji (taarifa binafsi)	
a. Jina la Kwanza na la Mwisho	
b. Nambari ya Simu	c. Nambari ya Rununu
d. Anwani ya Barua pepe	
e. Anwani ya Mahali Palipoathiriwa na Mkasa	
f. Nchi	g. Jiji, Jimbo, Msimbo wa Eneo
h. Anwani ya Mahali pa Sasa ikiwa ni Tofauti na Iliyo Hapo Juu	
i. Nchi	j. Jiji, Jimbo, Msimbo wa Eneo
k. Jina la Kampuni ya Bima	Nambari ya Simu ya Kampuni ya Bima
l. Taarifa za Mawasiliano Mbadala (jina na nambari ya simu)	
m. Idadi ya Jumla ya Watu Wazima katika Familia	Idadi ya Jumla ya Watoto katika Familia
n. Mapato ya Jumla ya Familia ya Kila Mwaka	

KUMBUKA: Lazima mapato ya kila mwaka ya familia yawe 200% au chini ya kiwango cha umaskini cha serikali kuu kwa familia ya ukubwa huo.

Miongozi ya Umaskini wa Taifa 2023

Ukubwa wa Familia	1	2	3	4	5	6	7	8
200% ya Kiwango cha Umaskini cha Serikali Kuu (mapato ya kila mwaka)	$29,160	$39,440	$49,720	$60,000	$70,280	$80,560	$90,840	$101,120

2. Taarifa za Upotezaji Makao

Nyumba ya Muda Mfupi – Familia inaweza kupokea hadi $5,000 kwa kupangisha nyumba kwenye makao yenye leseni kama vile hoteli au moteli, ikiwa nyumba ya familia imeharibiwa, haiwezi kukalika, haiwezi kufikika, au haipatikani kwa familia. Lazima stakabadhi ziwe kwa jina la meombaji.

Msaada wa Chakula – Ubadilishaji wa chakula kilichooza au kilichoharibika.

Mali Binafsi – Baadhi ya mifano ni: vyombo vya jikoni, usafi binafsi, mavazi, samani na vyombo vya chumba cha kulala, nk.

Matengenezo ya Nyumbani – Baadhi ya mifano ni: utengenezaji wa sehemu za jengo, utengenezaji wa sakafu, kuta, madari, milango, madirisha na mazulia. Msaada utakataliwa kutokana na mambo yafuatayo: hali zilizopo ndizo chanzo cha uharibifu; jengo linalomilikiwa na mwenye nyumba; na ikiwa hatimiliki ya jengo haiko kwa jina la mwombaji.

<table>
<tr><td>Tarehe ya Mkasa</td><td colspan="2">Aina ya Mkasa
☐ Kimbunga ☐ Mafuriko ☐ Nyingine:</td></tr>
<tr><td>Nyumba ya Muda Mfupi:
$</td><td>Msaada wa Chakula:
$</td><td rowspan="3">☐ Omba Fidia (jitayarishe kutoa stakabadhi)
☐ Omba Malipo ya Moja kwa Moja kwa Mkandarasi au Muuzaji Mwingine</td></tr>
<tr><td>Mali Binafsi:
$</td><td rowspan="2">Matengenezo ya Nyumbani:
$
Kumbuka: Lazima hatimiliki ya jengo liwe kwa jina la mwombaji.</td></tr>
<tr><td>Jumla Iliyoombwa:
$</td></tr>
</table>

3. Maelezo Mafupi ya Uharibifu Uliosababishwa na Mkasa na Uorodheshe Vitu Vilivyoharibiwa

4. Uthibitisho

☐ Ninathibitisha kwamba watu wanaopokea msaada katika familia ni wakazi halali wa Marekani.

☐ Ninathibitisha kwamba taarifa zilizotolewa kwenye fomu hii ni za kweli na sahihi. Ninaipa Iowa Department of Homeland Security and Emergency Management ("Idara") taarifa hizi za gharama kulingana na Iowa Individual Assistance Disaster Grant Program ("Mpango"). Ninaidhinisha Idara kuyapa mashirika yao ya msaada na mtu taarifa hizi kwa madhumuni ya kuendesha Mpango. Ninaelewa kwamba sistahiki fidia kulingana na Mpango, ikiwa nina bima inayofidia hasara zinazodaiwa, au ikiwa nimepokea msaada kutoka kwenye mipango mingine kwa vitu vilevile vinavyodaiwa, ninakubali kulipa Idara fedha zozote nilizopata kupitia Mpango huu ndani ya siku 60.

5. Tathmini mpya

Wewe au mtu anayekusaidia, anaweza kuomba tathmini mpya ikiwa hukubali hatua yoyote iliyochukuliwa dhidi ya ombi lako.

Ombi lako la tathmini mpya lazima likamilishwe ndani ya siku 30 kutoka tarehe iliyo kwenye barua ya kukataliwa.

Unaweza kuwasilisha ombi lako la maandishi kwa ajili ya tathmini mpya kwa kuwasilisha ombi lenye maelezo ya kina kwa:

Iowa Department of Homeland Security and Emergency Management
7900 Hickman Road
Suite 500
Windsor Heights, IA 50324

Au kupitia barua pepe kwa IndividualDisasterAssistance@iowa.gov

Ikiwa unahitaji msaada wa kuwasilisha ombi la tathmini mpya, mwombe wakili wako wa kesi ya mkasa.

6. Ubaguzi

Ni sera ya Iowa Department of Homeland Security and Emergency Management kumtendea kila mtu sawa wakati ajira na utoaji wa huduma kwa waombaji, waajiriwa na wateja bila kujali mbari, rangi, asili ya taifa, jinsia, dini, umri, ulemavu au hali ya kustaafu; hapa ikijulikana kama kategoria inayolindwa.

Ikiwa unahisi kwamba Iowa Department of Homeland Security and Emergency Management imekubagua au kukunyanyasa, tafadhali tuma barua inayoelezea kwa kina malalamishi yako kwa:

Iowa Department of Homeland Security and Emergency Management
7900 Hickman Road
Suite 500
Windsor Heights, IA 50324

Au kupitia barua pepe kwa IndividualDisasterAssistance@iowa.gov

Iowa Department of Homeland Security and Emergency Management ni mtoa huduma asiyebagua. Sera zinapatikana kwenye https://homelandsecurity.iowa.gov/policies.

Sahihi ya Mwombaji	Tarehe

Tafadhali wasilisha nyenzo zote za ombi kwa Community Action Agency yako ya karibu.

Pata shirika lako kwenye www.iowacommunityaction.org/find-an-agency. Mtu mwingine kutoka Community Action Agency yako ya karibu atawasiliana nawe ili kukagua ombi lako. Jitayarishe kutoa nyaraka zitakazoombwa.